TANGAZO LA SERIKALI NA. 895 la tarehe 1/11/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1)*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA KAWAWA YA MWAKA 2024

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa katika Eneo la Kawawa ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa Eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali litatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Jiji Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MIPAKA YA ENEO LA UPANGAJI

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KWW1 yenye majira - nukta 804069.48MS, 9297227.93KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS64$^0$MS kwa umbaliwa kilomita 0.770 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KWW2 yenye majira - nukta 804762.82MS, 9296891.42KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS35$^0$MG kwa umbali wa kilomita 1.054 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KWW3 yenye majira - nukta 804147.26MS, 9296035.38KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -

*Tangazo la Serikali Na. 895 (Linaendelea)*

Mashagharibi katika uelekeo wa KZ$67^0$MG kwa umbali wa kilomita 1.092 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KWW4 yenye majira – nukta 803137.16MS, 9296450.41KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ$50^0$MS kwa umbali wa kilomita 1.213 hadi ulipoanzia.

Dodoma,
28 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*